

JE, NI JINSI GANI UNAPASWA KUZUIA MAFUA?

Homa ya mafua ni tatizo la kila mwaka katika South Dakota—lakini uzuri ni kwamba si lazima kuipata kila mwaka. Unaweza kujilinda mwenyewe, wapendwa wako na jamii yako kwa kupata chanjo yako ya kimsimu.

JE, UKWELI NI GANI KUHUSU CHANJO YA MAFUA?



NI KWA AJILI YA UMRI MBALIMBALI.

Watoto kuanzia umri wa miezi sita wanapendekezwa kupata chanjo ya mafua ili kuzuia maradhi hayo. Kunazo chanjo ambazo zimependekezwa haswa kwa watu wenye umri wa miaka 65 au zaidi pia.



INAFANYA KAZI.

Chanjo hailindi dhidi ya kila aina ya mafua, lakini hupunguza kwa kiasi kikubwa uwezekano wa kuambukizwa, huzuia uwezekano wa kulazwa hospitalini na kukosa shule au kazi na hupunguza vifo vinavyohusishwa na mafua katika jamii za South Dakota.



INAPASWA KUCHUKULIWA KWA KILA MWAKA.

Aina za homa ya mafua hubadilika kila mwaka—kwa hivyo chanjo ya kila mwaka ndiyo njia bora ya kujilinda. Centers for Disease Control inapendekeza kupata chanjo yako mapema katika msimu kwa matokeo mema zaidi.



INAKUJA KWA NJIA NYINGI.

Sio chanjo zote za mafua hupeanwa kwa njia ya sindano. Kunazo chanjo za kufukiza puani kwa ajili ya watu walio na hitimu fulani za kimatibabu.



**Je, una wasiwasi kuhusu homa ya mafua?
Pata chanjo!
Tafuta jinsi ya kupata kituo cha chanjo
katika FluBug.org.**

